5000/=

PICHA

FORM NO._____

SHULE YA SEKONDARI MAIRIVA S.L.P 1722, ARUSHA

Simu: 0732 990701, 0754 314179, 0784 403511

NAMBA YA USAJILI: S.2380

FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2010/11

(*Fomu hii inatumika kwa kidato cha V hadi VI tu)*

1. **MAELEZO YA MWANAFUNZI (**Jaza nafasi zilizo wazi kwa herufi kubwa**)**

   a) Jina la mwanafunzi _____Jinsia_____

   b) Tarehe ya kuzaliwa:_____

   c) Dini_____Dhehebu_____

   d) Mwaka wa kumaliza kidato cha Nne: _____

   e) Kidato unachoombea nafasi_____

   f) Iwapo unahamia taja shule ya sekondari unayoihama_____

   (Ambatanisha cheti cha uhamisho na kumbukumbu nyingine muhimu)

   g) Jaza unahitaji nafasi ya BWENI AU KUTWA: _____

2. **MAELEZO YA MZAZI/MLEZI**

   a) Jina kamili la mzazi/mlezi:_____

   b) Anwani ya posta:_____

   c) Simu ya mzazi/mlezi:_____

   d) Mahali mzazi/mlezi anapoishi:

   Mkoa_____Wilaya_____

   e) Mwanafunzi anaishi na _____

   (chagua hapa chini:)

   - ✓ Baba na mama
   - ✓ Mama tu
   - ✓ Baba tu
   - ✓ Ndugu au jamaa

3. MAELEZO YA ELIMU

a) Shule uliyomaliza kidato cha nne:_____Mwaka:_____

b) Matokea ya mtihani wa taifa kidato cha nne: (Jaza gredi ulizopata)

B/ KPNG	KISW	CIVICS	GEO	HIST	PHYS	AGRICULT
B/ KNOWL	CHEM	COMM	MATHS	ENGL	BIOS	OTHER(S)

Pia ambatanisha hapa matokeo ya mtihani wako yaani *result slip* kutoka baraza la mitihani la Tanzania (NECTA).

4. MCHEPUO WA SHULE

Shule ina Combinations zifuatazo:

COMBINATIONS ZA SANAA/ARTS:

HISTORY, GEOGRAPHY AND LITERATURE **(HGL)**

HISTORY, KISWAHILI AND LITERATURE **(HKL)**

HISTORY, GEOGRAPHY AND KISWAHILI **(HGK)**

COMBINATIONS ZA BIASHARA:

ECONOMICS, COMMERCE, ACCOUNTANCY **(ECA)**

HISTORY, GEOGRAPHY, ECONOMICS **(HGE)**

ECONOMICS, GEOGRAPHY, MATHEMATICS **(EGM)**

COMBINATIONS ZA SAYANSI:

PHYSICS, CHEMISTRY, MATHEMATICS **(PCM)**

PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY **(PCB)**

CHEMISTRY, BIOLOGY, GEOGRAPHY **(CBG)**

PHYSICS, GEOGRAPHY MATHEMATICS **(PGM)**

5. CHAGUO LA MASOMO

Mwanafunzi atapendekeza “combination” tatu anazopenda kulingana na matokeo yake, shule itachagua moja kati ya hizo.

Chaguo la I ……..…

Chaguo la II ……

Chaguo la III……..…..……

Jambo la kuzingatia

1. Mwanafunzi anayejiunga na kidato cha 5 lazima awe na credits 3 au zaidi katika mitihani ya kidato cha nne kwa mujibu wa taratibu na kanuni za NECTA.

2. Iwapo mwanafunzi amemaliza miaka 4 au zaidi tangu awe na sifa za kufanya mtihani wa Taifa wa kidato cha VI hataruhusiwa kufanya mtihani huo kama mtahiniwa wa shule/School candidate. Hata hinyo Baraza la mitihani la Taifa halimzuii kufanya mtihani huo kama mtahiniwa wa kujitegemea/private candidate.

_____

Kwa matumizi ya ofisi tu:

Combination iliyothibitishwa na shule ni:_____

Jina la Mwalimu wa Taaluma: _____

Sahihi: _____

Tarehe: _____

6: ADA:

A: Combinations za Sanaa/Arts na Biashara

ADA KWA WANAFUNZI WA KUTWA

MAELEZO	MUHULA WA I	MUHULA WA II	JUMLA
Ada ya Usajili	100,000/=	-	100,000/=
Tahadhari	20,000/=	-	20,000/=
Ada ya shule	370,000/=	370,000/=	740,000/=
JUMLA	**490,000/=**	**370,000/=**	**860,000/=**

ADA KWA WANAFUNZI WA BWENI

MAELEZO	MUHULA WA I	MUHULA WA II	JUMLA
Ada ya Usajili	100,000/=	-	100,000/=
Tahadhari	20,000/=	-	20,000/=
Ada ya shule	495,000/=	495,000/=	990,000/=
JUMLA	**615,000/=**	**495,000/=**	**1,110,000/=**

B: Combinations za Sayansi

ADA KWA WANAFUNZI WA KUTWA

MAELEZO	MUHULA WA I	MUHULA WA II	JUMLA
Ada ya Usajili	100,000/=	-	100,000/=
Tahadhari	20,000/=	-	20,000/=
Ada ya shule	410,000/=	410,000/=	820,000/=
JUMLA	**530,000/=**	**410,000/=**	**940,000/=**

ADA KWA WANAFUNZI WA BWENI

MAELEZO	MUHULA WA I	MUHULA WA II	JUMLA
Ada ya Usajili	100,000/=	-	100,000/=
Tahadhari	20,000/=	-	20,000/=
Ada ya shule	550,000/=	550,000/=	1,100,000/=
JUMLA	**670,000/=**	**550,000/=**	**1,220,000/=**

C: MICHANGO YA WAJIBU (Siyo ya Hiari)

i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia shilingi elfu ishirini (20,000/=) tu kwa MWAKA kwa ajili ya shughuli za **MAHAFALI** ya kidato cha IV na VI yanayofanyika hapa shuleni mara mbili kwa mwaka.

ii) Kila mwanafunzi **MWISLAMU WA BWENI** anatakiwa kuchangia shilingi elfu ishirini tu (20,000/=) kwa MWAKA kwa ajili ya Futari/Daku wakati wa **MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI**.

iii) Kila mwanafunzi kwa MUHULA anatakiwa kuchangia **RIMU 2** za karatasi ya photokopi saizi ya A4 kwa ajili ya mitihani mwanafunzi anayoifanya kila wiki.

iv) Ada za mitihani ya Taifa ya Kidato cha II, IV na VI kama inavyotangazwa na Baraza ka Mitihani la Taifa (NECTA) kila mwaka

Karo na michango yote isipokuwa rimu ilipwe kupitia benki tu kwa kutumia jina na akaunti na ya shule. Baada ya kulipa njoo shuleni na 'pay in slip" nakala halisi/original' upewe risiti halali kwa malipo uliyofanya kule bank.

ANGALISHO:

- ✓ Akaunti ya shule ni **Mairiva Secondary School, CRDB -Arusha branch, Account No. 01j1034845300**
- ✓ Michango yote ilipwe sambamba na ada ya muhula wa kwanza
- ✓ Shule **haipokei** fedha **taslimu**/**cash** kwa sababu za kihasibu na za kiusalama.
- ✓ Mwanafunzi ambaye hajalipiwa ada/michango kamili hatapokelewa shuleni
- ✓ Rudisha fomu shuleni mara baada ya kuijaza
- ✓ **TUNASHAURI MWANAFUNZI WA A- LEVEL AKAE BWENI ILI AWEZE KUSOMA NA WENZAKE KATIKA MUDA USIO WA DARASANI.**

Baada ya kulipa ada wajibu wa shule kwa mwanafuzi ni pamoja na:

- ✓ Afundishwa na kumaliza silabasi
- ✓ Atalala kitandani peke yake
- ✓ Ataoga maji moto
- ✓ Atapewa chakula cha kufaa na cha kutosha
- ✓ Atashiriki shughuli za dini yake na michezo
- ✓ Atachungwa na kulelewa katika maadili mema

4. SARE MBALIMBALI

a) Sare ya shule kwa wavulana

1) Suruale mbili nyeusi za kitambaa, sio jeans wala kadet .
2) Mashati 2 rangi ya light blue ya mikono mifupi yasiyo na urembo wowote
3) Viatu vyeusi vya ngozi visiwe na kisigino kirefu
4) Sweta mbili rangi nyeusi na shingo ya “V”.
5) Soksi nyeusi zisizo na maua wala urembo wowote
6) Tai nyeusi isiyo na maua wala urembo wowote

b) Sare ya shule kwa wasichana

1) Sketi mbili nyeusi za marinda zinazofunika goti
2) Mashati 2 rangi ya light blue ya mikono mifupi yasiyo na urembo wowote.
3) Viatu vyeusi vya ngozi visiwe na kisigino kirefu
4) Sweta mbili rangi ya nyeusi na mikono mirefu, na shingo ya V”.
5) Soksi nyeupe ndefu (stockings) zisizo na maua wala urembo wowote.
6) Tai nyeusi isiyo na maua wala urembo wowote

c) Sare za bweni/nguo za kushindia na michezo kwa wavulana

1) Suruali jozi mbili za rangi ya bluu bahari
2) T-shirt jozi mbili za kijivu zisizo na maandishi au marembo yoyote
3) Truck suit isiyobana ya rangi ya kijivu yenye ufito/mstari mweupe miguuni na mikononi
4) Raba za michezo

d) Sare za bweni/nguo za kushindia na michezo kwa wasichana

1. Sketi jozi mbili za rangi ya bluu bahari zisizo na marinda wala kubana chini/tight
2. T-shirt mbili za rangi ya kijivu zisizo na maandishi au marembo yoyote
3. Truck suit isiyobana ya rangi ya kijivu yenye ufito/mstari mweupe miguuni na mikononi
4. Raba za michezo

e) Usukaji na Unyoaji kwa wote

1. Msuko wa nywele kwa wasichana ni “Utii wa Roda au twende kilioni” usio na madoido yoyote
2. Unyoaji ni wa nywele fupi zinazoruhusu njiti ya kiberiti kupenya ndani yake kwa wasichana na wavulana.

SARE ZOTE ZENYE SIFA ZIFUATAZO HAZIRUHUSIWI SHULENI AU BWENINI

i) Soksi fupi hususan kwa wasichana
ii) Suruale zinazobana, mlegezo/mnyonyo, zinazobana chini/chupa, zenye mshono wa “V” nyuma au zenye mifuko ya kubandika
iii) Sketi fupi zinazoacha magoti wazi na za mlegezo zenye belti kubwa zaidi ya sentimita 3
iv) Nguo za nyumbani ambazo sio sehemu ya sare za shule.
v) Mkanda wa kuvalia suruale wenye bakoli kubwa kuliko upana wa mkanda na wenye nembo/picha yoyote
vi) Usukaji au unyoaji wa mitindo mingineyo kama vile mdomo wa kuku, mzungu

Wa unga/kipara, mbenjuo, panki n.k. na madawa ya kubadili umbo asili la nywele, kama vile duke, perm, relaxer, curl, nk

5. VIFAA MBALIMBALI

a) Vifaa vya darasani

1. Daftari kubwa 9 na Daftari ndogo 4
2. Ruler, kalamu, pencil, rubber (kiasi cha kutosha)
3. Mathematical set 1 kwa wanaosoma Hesabu
4. Oxford Advanced learners' Dictionary 1kwa wanafunzi wanaosoma kiingereza
5. Flat file 1 la kuwekea mitihani kwa ajili ya marudio/revision
6. Begi la madaftri lisilo na maandishi au picha au marembo yoyote
7. Advanced level Pure Secondary Mathematics – 4^{th} edition by C.J Tranter kwa waosoma hesabu
8. Scientific Calculator kwa wanaosoma hesabu

b) Vifaa vya Bweni

1. Godoro 1 (ft $2^{1/2}$ x 4 x 6), Blanketi 1 na shuka 3 rangi ya bluu iliyokolea
2. Malapa, taulo, kitana/chana,
3. Sanduku imara la bati na kufuli mbili
4. Mwavuli mdogo 1
5. Ndoo 2 ndogo za kuogea/kufulia, brashi ya kuogea, dodoki,mswaki na dawa, n.k
6. Mto 1 na foronya 2 za bluu iliyokolea
7. Net 1 ya mbu yenye ngao
8. Sabuni za kufua, kuogea na mafuta ya kujipaka
9. Bakuli/sahani ya wastani na kikombe cha robo lita kwa ajili ya chakula/chai.
10. Khanga/kitenge jozi mbili (wasichana)
11. Nguo za ndani na za kulala/pajama

6. KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe 16/03/2010 saa 1.30 asubuhi. Wanafunzi wa bweni wanatakiwa kuripoti shuleni tarehe 15/03/2010 kabla ya saa 10.00 jioni.

7. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

A. TARATIBU KWA UJUMLA

1. Kuwahi shule na kuheshimu kengele daima
2. Hairuhusiwi kupiga kelele au kusababisha kero ya aina yeyote nje na ndani ya shule au darasani.
3. Kuwa katika sare kamili ya shule kila wakati
4. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka eneo la shule nyakati za masomo bila ruhusu ya maandishi kutoka kwa mwalimu wa zamu au mkuu wa shule
5. Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zake na za shule pia na kuujulisha uongozi wa shule iwapo kuna tatizo lolote katika mali hizo.
6. Tumia lugha ya heshima wakati wote. Lugha chafu au isiyo rasmi haikubaliki
7. Ugomvi wowote hauruhusiwi shuleni kwa wakati wowote.
8. Kuwa na adabu shuleni
9. Kuwa msafi usichafue ukuta
10. Takataka zisitupwe ovyo ovyo kwenye mazinigira
11. Hairuhusiwi kuchukua kitu chochote ambacho si chako
12. Hairuhusiwi kula au kunywa nyakati za masomo darasani
13. Heshimu waalimu, wakubwa na viranja
14. Heshimu kila mmoja uongo hauruhusiwi
15. Hairuhusiwi kukosa shule au bweni
16. Tumia na weka mazingira ya choo sawa sawa
17. Lugha ya mawasiliano ndani ya shule ni Kiingereza
18. Simama wakati wa kusalimu wakubwa
19. Simu za mkononi haziruhusiwi popote shuleni
20. Fedha zote za matumizi ziwekwe ofisini.

B. MAKOSA AMBAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

1. Kila aina ya wizi, iwe wa kutumia nguvu au udanganyifu
2. Kila aina ya tabia inayohusiana na mapenzi
3. Uvutaji wa sigara na madawa ya kulevya
4. Wizi wa mitihani (Pia kuibia mwingine darasani)
5. Aina yoyote ya uonevu kwa mwingine
6. Kutumia lugha chafu kwa wafanyakazi wa shule au mwanafunzi mwingine
7. Kuruka ukuta au uzio kutoka nje au ndani ya shule
8. Kuharibu makusudi mali ya shule, au ya mwenzako
9. Kutoa mimba
10. Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito kwa mwanafunzi
11. Kutoroka shuleni
12. Kuingia katika majumba ya starehe
13. Kuchelewa kufika shuleni siku ya kufungua shule siku mbili au zaidi kunaweza kusababisha kufukuzwa au kubaki shuleni wakati wa likizo kwa gharama ya mzazi.

C. SHERIA ZA BWENI

1. Zungumza lugha ya kiingereza wakati wowote
2. Kupiga kelele hairuhusiwi
3. Dumisha usafi bwenini
4. Tandika kitanda chako na kuhakikisha ni kisafi daima
5. Hakikisha mabomba ya maji yamefungwa na hayatoi maji ovyo. Pia hakikisha taa zote zimezimwa pale ambapo hazihitajiki kwa wakati huo.
6. Weka vifaa vyako kwenye begi na sanduku lako
7. Usitundike nguo zako ukutani , kitandani au madirisha
8. Weka viatu vyako kwa mpangilio chini ya kitanda chako
9. Lala kwenye kitanda ulichopewa tu na siyo vinginevyo
10. Redio haziruhusiwi bwenini
11. Simu za mkononi (mobile phones) haziruhusiwi shuleni/bwenini
12. Mawasiliano na watu wengine nje ya bweni hayaruhusiwi
13. Vaa nguo za heshima uwapo bwenini na hasa nguo zilizoruhusiwa
14. Mapambo na vitu vingine kama mikufu, shanga nk haviruhusiwi
15. Hairuhusiwi kuandika maandishi yoyote ukutani.
16. Hairuhusiwi kununua vyakula vya aina yoyote kutoka nje ya maeneo yanayolizunguka bweni
17. Lugha ya matusi hairuhusiwi ndani na nje ya bweni
18. Wizi wa aina yoyote hauruhusiwi bwenini
19. Hairuhusiwi kunywa kileo cha aina yoyote, kuvuta sigara au madawa ya kulevya.
20. Hairuhusiwi kuvunja au kuharibu kitu chochotekilicho mali ya bweni (shule)
21. Hairuhusiwi kulala bwenini kwa kuumwa bila kibali cha matron au patron wa shule.

ANGALISHO

- ✓ Sheria hizi zimetungwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mujibu wa Wizara ya Elimu.

- ✓ Pia sheria zote zinalenga katika kumjenga mwanafunzi kiakili na kimaadili ili hatimaye aweze kulitumikia Taifa kwa uadilifu na kuwa raia mwema.

- ✓ Sheria nyingi za bweni hutungwa kufuatana na sheria za nchi. Aidha baadhi ya sheria hutungwa kwa kuzingatia mazingira ya shule na kanuni za wizara ya Elimu zinazohusu uendeshaji wa Shule za Sekondari. Kila mwanafunzi anapaswa kuzisoma na kuzielewa sheria hizo kwa nia ya kuzifuata.

- ✓ Uvunjaji wa sheria za shule unaweza kusababisha mwanafunzi kupewa adhabu au kufukuzwa shule

- ✓ Utii wa kengele ni jambo muhimu sana kila mwanafunzi azingatie

- ✓ Hakuna mjadala wowote wa wanafunzi utakaokubalika wenye nia ya kubadili au kupindisha sheria hizi zenye lengo la kuleta amani na utulivu shuleni.

8. FOMU YA KUPIMA AFYA

Fomu hii ijazwena daktari baada ya kupima afya ya mwanafunzi.

MAIRIVA SECONDARY SCHOOL P. O BOX 1722, ARUSHA

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officer in respect of all new students:

Student's Full Name_____
Age: _____
Gender: _____
Blood count (Red and white Blood cells) _____
Stool examination_____
Urinalysis_____
Typhoid fever_____
T.B _____
Eye test_____
Ears test_____
Chest_____
Spleen_____

Additional information: e.g. Physical defects or impairments, infections, Chronic or family disease, etc_____
_____

Healthy problems which need consideration e.g. Asthma

_____
_____

I certify that the above is **FIT**/ **UNFIT** to pursue further education as stated above:

Signature: ----------

Designation: ----------

Station: ---------- Date: ----------

(Rudisha fomu hii shuleni mara baada ya kijazwa na daktari)

9. UTHIBITISHO WA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE

(Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi)

Mimi _____

iwapo nitachaguliwa kujiunga na shule hii, ninahaidi kufuata sheria, masharti na kanuni zote zitakazotolewa na uongozi wa shule wakati wote niwapo shuleni.

Sahihi ya mwanafunzi: _____ Tarehe: _____

(Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi)

Mimi _____,

mzazi/mlezi wa _____

iwapo mwanangu atachaguliwa kujiunga na shule hii ninahaidi kutoa ushirikiano kwa walimu pamoja na uongozi mzima wa shule katika kumlea mtoto katika maadili yanayopasa. Ninahaidi pia kulipa ada na michango yote itakayojitokeza katika shule hii kwa wakati upasao.

Sahihi ya mzazi/mlezi:_____ Tarehe: _____